TANGAZO LA SERIKALI NA. 545 la tarehe 5/7/2024

SHERIA YA MISITU
(SURA YA 323)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29(1))*

AMRI YA KUTANGAZA MSITU WA HIFADHI YA MAZINGIRA ASILIA ITULU HILL YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Itulu Hill ya Mwaka 2024.

Tangazo

2. Eneo la hifadhi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Itulu Hill.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA SIKONGE


MSITU WA HIFADHI YA MAZINGIRA ASILIA ITULU HILL

*Makadirio ya Eneo:* Hekta 403625.62 au Kilometa za Mraba 4036.26

Unakopatikana na Mipaka

Eneo lote la ardhi iliyohifadhiwa awali chini ya Msitu wa Hifadhi Ituli Hill linalopatikana Wilaya ya Sikonge, Mkoa wa Tabora kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Jb 2751 ya mwaka 2018 (Skeli 1:100,000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na lenye mipaka ifuatayo:

*Tangazo La Serikali Na. 545 (Linaendelea)*




Dodoma, <br>
___24 Mei, 2024

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI <br>
*Waziri wa Maliasili na Utalii*